

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

*Dodoma
21 Oktoba, 2023*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
RAIS SAMIA ATOA SALAMU ZA RAMBIRAMBI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ametuma salamu za rambirambi kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balози Dkt. Batilda Salha Burian kufuatia vifo vya watu 18 vilivyotokea katika ajali ya gari.

Ajali hiyo imetokea leo saa 5 asubuhi katika kata ya Uchama, tarafa ya Nyasa wilaya ya Nzega mkoani humo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora ACP Richard Abwao waliopoteza maisha ni wanaume 14 akiwemo mtoto mmoja na wanawake 4.

Majeruhi ni 60 ambapo majeruhi 31 wanatibiwa Hospitali ya Wilaya ya Nzega, 19 wako Hospitali ya Rufaa ya Nkinga, 1 anatibiwa Hospitali ya Rufaa ya Bugando na 9 wametibiwa na kuruhusiwa.

ACP Abwao amesema ajali hiyo imehusisha basi la kampuni ya Alfa lililokuwa likisafiri kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam ambalo liligongana na Lori la mafuta lililokuwa likitoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza.

Rais Samia anawapa pole majeruhi wa ajali hiyo pamoja na wafiwa wote na anaungana na familia hizo katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.

Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema Peponi. Amina.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu